Swahili

## Karatasi ya ukweli

# Wanawake na Kaswende



Kaswende ni maambukizo makubwa na wanawake wengi zaidi nchini Australia wanaipata. Jifunza kuhusu kaswende na jinsi unavyoweza kujikinga.

**Kaswende** ni maambukizo ya zinaa (STI) ambayo yanaambukizwa kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine wakati wa kujamiana.

### Wanawake wengi zaidi wenye umri wa miaka 15 hadi 44 wanaipata

Kati ya miaka 2016 na 2022 viwango vya kaswende ya kuambukiza katika wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 44 viliongeza kwa asilimia 158 nchini Australia*.

### Huenda usijue una kaswende

Watu wengine wanaweza wasijisikie kuwa wanaumwa au hawajui kuwa wana kaswende. Inawezekana kuwa na kaswende na kumwambukiza mpenzi wako bila kujua.

Tulipendekeza kuwa wewe na mpenzi wako mpate kipimo kamili cha STI mara kwa mara –hata kama huna dalili zozote.

Kama ukigundua kuwa una kaswende, umjulishe mpenzi wako ili aweze pia kupimwa na kutibiwa. Hii itazuia kaswende kuweza kurudi kwako au kuwaambukiza wengine.

### Dalili za kaswende ni tofauti kati ya mtu na mtu

Kama ukiambukizwa kaswende, dalili za kwanza ni vidonda au donda kwenye sehemu za siri, mkundu na mdomoni.

**Baada ya muda dalili zingine zinaonekana:**

- Upele
- Vidonda vya ngozi
- Tezi za limfu zilizovimba
- Kupoteza nywele
- Maumivu ya misuli na viungo
- Maumivu ya kichwa
- Uchovu

### Bila matibabu, kaswende inaweza kusababisha:

- Maambukizo ya ubongo
- Shida ya akili
- Kushindwa kwa mapafu na moyo
- Upofu
- Kifo

*Idara ya Afya na Matunzo ya Wazee ya Australia, (2023), Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Magonjwa Yanayoarifiwa. Inapatikana kwa https://nindss.health.gov.au/pbi-dashboard

MULTICULTURAL HIV & HEPATITIS SERVICE

**Wilaya ya Afya ya Mahali ya Sydney ya Kusini Magharibi**
Huduma ya Kukuza Afya

NSW GOVERNMENT

Karatasi ya ukweli

# Wanawake na Kaswende

## Kuambukiza kaswende kwa mtoto wako kunaweza kusababisha kifo

Ikiwa una kaswende na uko mjamzito, unaweza kuambukiza mtoto wako kabla ya kuzaliwa.

**Hii inajulikana kama kaswende ya kuzaliwa na inaweza kusababisha:**

- kuharibika kwa mimba
- kifo kabla ya mtoto kuzaliwa
- kuzaliwa mapema
- uzito mdogo wa kuzaliwa
- kifo cha mtoto muda mfupi baada ya kuzaliwa

Kaswende ya kuzaliwa inaweza kusababisha uharibifu wa kudumu wa ubongo au kiungo kwa mtoto wako. Hii inaweza kuathiri ukuaji na maendeleo yake.

Watoto wachanga wengine wanaweza kutoonyesha shida za kukua na maendeleo hadi wanapokuwa wakubwa zaidi kusababisha utambuzi uliochelewa.

## Kupata kipimo cha kawaida kunaweza kukusaidia

Tunapendekeza kuwa upate kipimo kamili cha STI mara kwa mara – hata kama huna dalili zozote na haswa kama wewe ni mjamzito au unapanga kuwa mjamzito.

Vipimo vya kaswende ni vipimo muhimu vya kawaida wakati wa ujauzito.

Utapimwa angalau mara mbili wakati wa ujauzito wako ili kuzuia kaswende ya kuzaliwa. Hii ni kwa sababu kaswende imeongezeka katika jamii. Kipimo kingine cha kaswende kinaweza kufanyika ikiwa una uwezekano mkubwa wa kuipata.

Tembelea daktari yako, mkunga au mtoaji huduma wa akina mama ili kupata kipimo kamili cha STI, ikijumuisha kipimo cha kaswende.

## Matibabu ni rahisi

Matibabu ya kaswende ni rahisi. Dawa (kwa kawaida kupita sindano) huondoa maambukizo na ni salama kwako na kwa mtoto wako.

Utahitaji kufanya vipimo vya damu baada ya matibabu yako kuangalia kwamba yamefanya kazi

Daktari yako au mtaalamu wa afya ya kingono anaweza kukutiba na kukufuatilia

## Jinsi ya kuzuia kaswende

**Njia nzuri sana ya kuzuia kaswende ni kufanya ngono salama:**

- Kila wakati tumia kondomu na mpenzi mpya na vilainishi vya salama kwa kondomu (k.m. vyenye maji au vya silikoni).
- Epuka kufanya ngono na mtu ambaye ana kidonda au donda kwenye sehemu zake za siri, mkundu au mdomo.
- Pata vipimo vya STI kwa kawaida ambavyo vinajumuisha kaswende.
- Wapenzi pia wanapaswa kupimwa (na kutibwa) mara kwa mara ili kuzuia kaswende kurudi kwako au kuwaambukiza wengine.
- Ikiwa hujisikii vizuri kuwasiliana na wapenzi wewe mwenyewe, unaweza kutembelea kwa **www.letthemknow.org.au** ili kupata ushauri au zungumza na daktari yako.

**Changanua msimbo wa QR ili kujua zaidi kuhusu kaswende na afya ya wanawake.**

MULTICULTURAL HIV & HEPATITIS SERVICE

**Wilaya ya Afya ya Mahali ya Sydney ya Kusini Magharibi**
Huduma ya Kukuza Afya

NSW GOVERNMENT